Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Pili – Tarehe 10 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta ) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na 10

**Athari ya Rushwa katika Utawala Bora wa Taifa**

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa,vitabu vya Utandawazi vinavyoongelea athari za Rushwa ulimwenguni kikiwemo kile kilichoandikwa na Charles *W.L. Hill* wa *Washington University* vinaonyesha jinsi rushwa inavyoathiri Utawala Bora wa Taifa kwa kiwango kikubwa; na kwa kuwa utafiti uliofanywa mwaka 2001 kuhusu rushwa ndani ya Serikali 91 zilizohusishwa imeonyesha kuwa nchi kama Finland na Canada zinaongoza kwa kuwa na Utawala Bora kwa kutokuwa na rushwa ndani ya Serikali zao; na Russia, Indonesia na Nigeria zilionekana kukithiri kwa rushwa Serikalini lakini Bangladesh ikiwa ya kwanza kuwa na Serikali iliyokithiri kwa rushwa kubwa kubwa na kutokuwa na sifa ya nchi inayosimamia Utawala Bora:-

Je, Serikali ya Tanzania ambayo haikuwepo katika orodha ya nchi hizo 91 zilizofanyiwa utafiti, inafanya jitihada zipi ili iwe na sura ya usafi kama Finland na Canada?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi ya Finland na Canada zinafanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa na kwamba nchi hizo zinashika nafasi za juu Duniani na zinazidi nchi yetu ya Tanzania katika tafiti mbalimbali zilizofanyika. Hizi ni nchi zenye uchumi imara duniani, zimeendelea kiviwanda na kibiashara, watumishi wa umma na wananchi wanalipwa vizuri sana na kupewa marupurupu mazuri, hatua ambayo bado hatujaifikia.

Pia demokrasia kwenye nchi hizi imekuwepo muda mrefu, imekomaa na kuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna jitihada nyingi ambazo nchi yetu imefanya katika mapambano dhidi ya rushwa. Katika kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mbunge wa Same Mashariki). Ni vyema tukatambua jitihada ambazo nchi yetu imefanya katika mapambano dhidi ya rushwa.

Nchi yetu imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa kupambana na Rushwa (*United Nations Convention Against Corruption*); Mkataba ambao unatuwezesha kushirikiana na nchi mbalimbali duniani katika jitihada zetu za kupambana na rushwa. Mwaka 2007 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Hii ni sheria ambayo imepanua wigo wa makosa yanayohusiana na rushwa na tuna imani kwamba, itatoa mchango mkubwa katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hivi sasa inatekeleza awamu ya pili ya Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa (*NACAP* II). Kwa hiyo tunaamini mpaka sasa tuko kwenye njia sahihi katika mapambano yake dhidi ya rushwa.

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Kimataifa ya ‘‘*Transparency International*’’ umeonyesha kwamba alama ambazo Tanzania imekuwa ikipata zimeongezeka, kutoka 2.2 mwaka 2001 na kufikia 3.2 mwaka 2008 na kuifanya nchi yetu kuwa ya kwanza kwa kuwa na kiwango kidogo cha rushwa katika nchi za Afrika ya Mashariki.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tafiti mbalimbali za viwango vya rushwa duniani zinazofanywa na mashirika tofauti zimekuwa na matokeo yanayokinzana kuhusiana na hali ya rushwa kwenye nchi mbalimbali. Kwenye ripoti ya *Transparency International* ya mwaka 2005, Canada ilishika nafasi ya 14 ikiwa na alama 8.4 na mwaka 2008 Finland imetajwa kwenye ripoti ya *Transparency International* kushika nafasi ya 5 duniani ikiwa na alama 9.0 wakati Canada imetajwa kushika nafasi ya 9 duniani ikiwa na alama 8.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi yetu ya kupunguza rushwa na kuifanya nchi yetu iwe na sura ya usafi kama Finland na Canada na nchi nyingine zenye kiasi kidogo cha rushwa, tunatakiwa kuendelea na mikakati yetu tuliyojiwekea ya kuzuia na

kupambana na rushwa nchini. Serikali inachukua hatua kali pale watendaji wake wanapobainika kuwa wametenda vitendo vya kukiuka maadili vikiwemo vya kujihusisha na rushwa.

Hatua za kiutawala ziendelee kuchukuliwa kwa watuhumiwa pale ambapo ushahidi wa kutosheleza hatua za kimahakama haupo.

Mheshimiwa Spika, mahakama zetu zitoe adhabu kali kwa wale watakaopatikana na na hatia ya kuomba na kupokea rushwa kama sheria inavyoelekeza. Ni muhimu sana mahakama zetu ziwe ni mahali ambapo haki haiuzwi wala kununuliwa kwa gharama yoyote. Kwa maana nyingine ziwe mahali ambapo rushwa haipo kabisa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waendelee kukemea vitendo vya rushwa na kuibana Serikali pale ambapo imelegalega katika mapambano dhidi ya rushwa. Bunge liendelee kutunga sheria ambazo zina vipengele ambavyo vinazuia rushwa katika nyanja zote. Ni muhimu sana kwa Wabunge kuwa wasafi na wasiojihusha na vitendo vya rushwa, hata kwa kuhisiwa tu.

Mheshimiwa Spika, mihimili ya dola ni muhimu sana katika mapambano dhidi ya rushwa. Lakini bila kuwahusisha wananchi wote wa Tanzania itakuwa vigumu kupata mafanikio makubwa katika mapambano haya. Ni muhimu jitihada za kuwahusisha wananchi wote katika mapambano haya ziendelee na pia kutumia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, tuendeleze mapambano dhidi ya rushwa kwa dhati na tuongezee utashi wa kisiasa katika mapambano haya.

Kwa mkakati huo, nchi yetu itakuwa safi na kupata sifa duniani kama nchi za Finland na Canada ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja katika swali lake.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali madogo ya nyongeza:-

Kwa kuwa utashi wa kisiasa wa kupambana na vita dhidi ya rushwa unaweza pia kupimwa na hatua zinazochukuliwa dhidi ya wale ambao wamekuwa wakituhumiwa katika mchezo huu mchafu wa rushwa.

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu kuchukua hatua za haraka kuwafikisha Mahakamani wale wote ambao wamehusika kwa namna moja ama nyingine kwenye mikataba ambayo ina harufu ya rushwa ikiwemo ya *Richmond*, *IPTL*, *EPA* na mengine ambayo haiiweki nchi yetu katika sura nzuri katika uso wa dunia?

(b) Kwa kuwa kumekuwepo na dalili kwamba mikataba kama ya Madini na mikataba mbalimbali ambayo Serikali yetu imekuwa ikiingia baadaye ndiyo tunakuja kugundua kwamba kuna harufu ya rushwa katika mikataba hiyo:-

Je, ndiyo tuseme kwamba katika Taasisi muhimu kama *BOT* na katika kuingia mikataba hiyo Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa au *PCCB* haipo katika Benki Kuu kiasi kwamba inaweza kutokea ufisadi kama ule uliotokea? Pengine labda niweke vizuri swali hili Mheshimiwa Spika.

Pengine tunachukua hatua gani za kukinga badala ya kuhangaika kutibu ili tuiweke nchi yetu katika sura nzuri katika uso wa dunia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Ole-sendeka, kwa maswali yake na naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

Kuhusu hatua zinazochukuliwa kuwafikisha Mahakamani wale wote waliohusika na kesi mbalimbali nadhani yeye anatambua kwamba Serikali inafutia kesi zote hizi kwa karibu sana lakini ufuatiliaji wa kesi mbalimbali za rushwa unaongozwa na Sheria ya rushwa ambayo inakataza kabisa kuzungumzia mwenendo wa uchunguzi wa kesi yoyote.

Kuzungumzia mwenendo wowote wa kesi kabla haijafika Mahakamani na hata ikifika Mahakamani ni kosa la jinai. Kwa hiyo, kwa hapa sitoweza kumpa majibu kwamba tumefikia wapi na kesi ya *IPTL* na *EPA*. *EPA* iko Mahakamani na yeye anatambua hiyo. Siwezi kuzungumzia *Richmond* hiyo iko katika hatua mbalimbali na kwa kiasi kikubwa anaelewa kwamba masuala ya *Richmond* yamekuwa kidogo yana utata kutokana na kwamba *Richmond* wenyewe katika mchakato mzima hawakupata hata senti Tano. Haijalipwa, kwa hiyo hakuna hata pesa ambayo imepita na kwenye rushwa lazima kuonyesha *Consideration* ambayo imetolewa katika *parties* ambazo zinahusikana na rushwa. Kwa hiyo, bado tuna kitendawili ambacho tunaendelea kukishughulikia na siwezi katika hatua hii kuzungumzia masuala haya.

Mheshimiwa Spika. Swali lake la pili anazungumzia mikakati kuhusu mikataba mbalimbali ambayo inaingiwa na Benki Kuu na vyombo vyetu vingine. Ni kweli sote tunafahamu kwamba, wenzetu ambao walipewa dhamana ya kuingia mikataba mbalimbali walikuwa hawana utaalamu wa kutosha na hivyo kutuingiza katika matatizo makubwa. Lakini Serikali inachukua kila hatua ya kuhakikisha kwamba matatizo haya ya kuingia kwenye mikataba ambayo haina manufaa na nchi yetu yanapewa Wataalamu ambao kwa sasa Serikali inafanya jitihada ya kutoa mafunzo ya kiutaalamu jinsi ya kuingia katika mikataba hii. Nashukuru.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika ahsante, hivi karibuni nimesoma katika gazeti, Rais alipata orodha ya wala rushwa *TRA*, alichukua taarifa hiyo akampelekea Kamishina Mkuu wa *TRA*. Je, huo ndio utashi wa kisiasa, ndio utaratibu unaotaka kutumika hivi sasa, kwamba Rais anapopata taarifa ya wala rushwa anakipelekea kile kile chombo ambacho kinatuhumiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, kama ifuatavyo;

Taarifa ulizopata zilizotoka kwenye magazeti kwa kweli mimi siwezi kuzizungumzia taarifa zilizotoka kwenye magazeti kwa sababu sina uhakika wa hayo ambayo yamezungumzwa na magazeti, kama tunavyojua magazeti yetu siku hizi mengi huwa yanapotosha. (*Makofi*)

Na. 11

**Ufanisi wa Mbunge kuwa na Nyadhifa Mbili**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini juu ya ufanisi wa utendaji wa Mbunge aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au kuwa Waziri?.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shams Faki, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo ndiyo Sheria mama inayoongoza nchi hii, Ibara ya 36(1) (2) inampa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka na kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya uongozi mbalimbali katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Hivyo kwa mantiki hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawezi kuingiliwa katika uamuzi wake wa kumteua Mbunge kuwa Waziri au Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Rais kufanya uteuzi humkabidhi mteuliwa nyaraka, miongozo mbalimbali ya utendaji na maelezo mahsusi *( job description)* ya majukumu yake na ya Taasisi anayoiongoza. Maelezo haya humsaidia mteuliwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi na kuwajibika ipasavyo kulingana na nafasi aliyopewa.

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia uwezekano wa kukosekana kwa ufanisi wa Wabunge wanaoteuliwa kushika madaraka ya Uwaziri au Ukuu wa Mkoa, Serikali imeweka utaratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa wateuliwa hao na kuweka mipaka ya kiutendaji katika majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Wabunge ambao wametakiwa kushika nafasi za Uwaziri au Ukuu wa Mikoa wamedhihirisha kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi na ufanisi mkubwa.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna hoja ya kutenganisha utendaji wa shughuli za Bunge na zile za Serikali, kwa kuepuka kuteuliwa Mbunge kuwa Waziri au Mkuu wa Mkoa, na kwa kuwa Mbunge kuteuliwa kuwa Waziri au Mkuu wa Mkoa kunaleta mwingiliano wa maslahi. Jambo ambalo ni kinyume na utawala bora:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu hoja hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Faki swali lake, kuhusu hoja ya kutenganisha nafasi hizi. Nafasi alizozitaja zote ni *Political Posts* sasa sijui anazungumzia nafasi ipi?

Na. 12

**Gharama ya Zoezi la Sensa ya Mwaka 2012**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inatarajia kuendesha zoezi la sensa mwaka 2012 na kwamba zoezi hilo lina umuhimu wa kipekee katika kusaidia Serikali kupanga mipango yake ya maendeleo kwa wananchi wake:-

(a) Je, zoezi hili litagharimu shilingi ngapi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema ikawatumia Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kuendesha zoezi hilo, ili kupunguza gharama zitakazotumika kuajiri watu, kuwapa mafunzo, ununuzi wa magari, vifaa na posho za kujikimu?

(c) Je, kwa nini Serikali isiazime magari kutoka katika Idara zake mbalimbali katika kuendesha zoezi hilo ili kuepuka gharama kubwa ya ununuzi wa magari?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zoezi zima la sensa tangu maandalizi, ukusanyaji na utoaji wa taarifa kwa umma na watumiaji wengine ni mchakato wa muda wa miaka ipatayo saba. Katika kila hatua ya sensa, shughuli mbalimbali hufanyika na kila hatua huhitaji mafunzo, utaalamu na vitendea kazi vya aina mbalimbali. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa zoezi la sensa lina umuhimu wa kipekee katika kusaidia Serikali kupanga mipango yake ya maendeleo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi itakayofanyika nchini mwezi Agosti, 2012 inatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 113.7. Kiasi hiki cha fedha kitatumika kwa kipindi cha miaka takribani saba kuanzia mwaka wa fedha wa 2008/2009 hadi mwaka 2014/2015.

(b) Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi ni zoezi shirikishi, ambalo hushirikisha watendaji kutoka Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na wao wana majukumu yao katika maandalizi, pamoja na ukusanyaji wa taarifa za sensa; na wao pia watajumuishwa kwenye mafunzo yatakayohitajika.

Jukumu kubwa la viongozi hawa wakati wa zoezi la kuhesabu watu ni kuhakikisha kuwa kila mtu kwenye eneo lake la utawala anahesabiwa na anahesabiwa mara moja tu.

Kazi ya ukusanyaji wa takwimu inahitaji taaluma, kwani sensa sio kuhesabu watu tu, bali pia ni kukusanya taarifa nyingine zitakazotoa viashiria mbalimbali vitakavyosaidia katika kutathimini na kupanga mipango ya maendeleo.

(c)Mheshimiwa Spika, wakati wa kufanya zoezi la sensa mwezi Agosti mwaka 2012 pamoja na mikakati mingine, Serikali itaweka utaratibu wa kuazima magari kutoka idara mbalimbali za Serikali. Utaratibu wa kuazima magari hautakuwa mpya, ulitumika wakati wa sensa ya mwaka 1967, 1978, 1988 na 2002.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na naishukuru Serikali na kuipongeza kwa sasa kuwajumuisha Wenyeviti ambao ndio wanaojua watu wao katika maeneo yao.

Je, malipo au posho ya Wenyeviti hawa itajulikana mapema ili Wenyeviti hao wajue?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavyo.

Kila mtendaji katika sensa ana wajibu wa kupata posho kulingana na shughuli yake, wakati utakapofika tutatoa taarifa ni posho kiasi gani ambayo kila mtendaji atatakiwa kupatiwa.

Na. 13

**Kutokomeza Mila za Ukeketaji na Watoto wa Kike Kuolewa Katika Umri Mdogo**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hapa nchini zipo mila na desturi ambazo kwa sasa zinaonekana kupitwa sana na wakati, mfano vitendo vya ukeketaji na watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo na kwa kuwa mila hizi zimeleta madhara makubwa katika Wilaya ya Serengeti na Tarime Mkoani Mara, kwa kupunguza idadi ya watoto wa kike katika shule za sekondari:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza wimbi la watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo?

(b) Kwa kuwa ukeketaji husababisha madhara mengi sana kama vile fistula na matatizo ya kujifungua. Je, Serikali imejiandaa vipi kutoa elimu juu ya athari zinazotokana na ukeketaji katika Wilaya hizo?

(c) Kutokana na idadi ya watoto wa kike kupungua sana shuleni katika Wilaya hizo kutokana na mila potofu za kuwaoza bado wadogo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza nafasi za watoto wa kike katika sekondari sanjari na watoto wa kiume?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba kumjibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba zipo mila na desturi kwa sasa zinaonekana kupitwa na wakati na zinazoendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake kwa mfano, ukeketaji na kuolewa katika umri mdogo pamoja na athari zake.

Aidha, Serikali ina mikakati mbalimbali ya kupunguza wimbi la watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo. Mikakati hiyo ni pamoja na utekelezaji wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake ambayo inatamka wazi kwamba, ni mwiko kuoza mwanafunzi pamoja na kuainisha adhabu kwa yoyote anayehusika na kosa hilo.

Vile vile Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuandaa sheria moja ya mtoto ambayo itakamilishwa na kuletwa katika Bunge lako Tukufu wakati wowote kuanzia sasa. Mikakati mingine ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998 na mamlaka waliyopewa Serikali za Mitaa ya kutunga sheria ndogo ndogo

watakazoona zinafaa katika kuleta Maendeleo na Ustawi katika Halmashauri zao. Hivyo tunashauri Halmashauri kutunga sheria zitakazosaidia kutatua tatizo hili katika maeneo yao.

(b)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ukeketaji husababisha madhara mengi wakati wa kujifungua pamoja na athari zake kwa mfano fistula, Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mkakati wa taifa wa mwaka 2001 – 2015 wa kutokomeza ukeketaji ambao lengo lake ni kupunguza au kuondoa kabisa ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike.

Aidha, Wizara yangu ina mpango wa kuendeleza kampeni ya Kataa Ukatilii Dhidi ya Wanawake na Watoto iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais mwaka jana. Mpango huu utatekelezwa kwa awamu kwa kuanzia kanda ya Ziwa, hivyo itajumuisha Wilaya za Serengeti na Tarime alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua athari za mila potofu dhidi ya maendeleo ya elimu ya watoto wa kike, imechukua hatua za makusudi za kuhakikisha uwepo wa fursa sawa ya elimu ya sekondari kwa watoto wa kike na wavulana.

Hatua hizo ni pamoja na uteuzi sawa kati ya wasichana na wavulana wa kuingia Kidato cha Kwanza, kuhamasisha ujenzi wa mabweni/hosteli kwa ajili ya wasichana na kwa sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ipo katika mchakato ambao unaelekea kutafuta ufumbuzi wa kuwarejesha masomoni wanaopata mimba wakiwa shuleni.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini bado ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Sheria aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, Sheria ya Elimu, haijaonyesha kiwango kikubwa katika kumkomboa mtoto wa kike kutokana na janga hili na kwa kuwa amekiri kwamba kuna Sheria zitarekebishwa ambapo hajatueleza ni lini Sheria hizo zitaletwa hapa Bungeni, sasa mimi nina swali moja.

Je, ni mkakati gani wa dharura Wizara hii itachukua katika kukabiliana na janga hili, hasa wilayani Serengeti, Tarime na maeneo mengine yoyote Tanzania yaliyoathirika na janga hili la ukeketaji?

Lakini suala la pili, kwa kuwa zoezi zima la upigaji kura kwa siri dhidi ya wauaji wa walemavu wa ngozi limeonyesha dalili nzuri. Sasa ni kwanini zoezi hilihili la upigaji kura kwa siri lisitumike katika maeneo haya ya Tarime na Serengeti ili kuwakamata Mangariba wote wanaofanya zoezi hili la ukeketaji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii , Jinsia na Watoto, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosemary Kirigini, kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 bado inakuwa kwamba haitekelezwi vizuri. Haitekelezwi vizuri kwa sababu kuna matatizo kwamba, Sheria nyingi bado wananchi hawajazifahamu. Na la pili ambalo linafanya hiyo Sheria isiweze kutekelezeka vizuri ni matatizo yetu ya mila na desturi kwamba, mtoto wa kike anaonekana kwamba ni mtu wa kuolewa tu kwa hiyo akipewa mimba wazazi wanakwenda kuingia mikataba na yule aliyempa mimba pamoja na uongozi wa Serikali ambao uko kwenye *grass root* wanahakikisha kwamba wanawapatanisha, kwa hiyo Sheria haichukui mkondo wake.

Kwa hiyo, nachoona hapa ni kwamba sisi kama Wizara tumeanza kujipanga baada ya kuzindua hii kampeni mwaka jana mwezi Mei, ya Kataa Ukatili dhidi ya Wanawake, tumejipanga sasa tumetengeneza mpango ambao tunauanzia kwenye Kanda ya Ziwa ambako kuna matatizo mengi na tumeishapata gari la sinema la kuendeleza hiyo elimu katika Kanda ya Ziwa na tukimaliza tutaendelea kwenye Kanda nyingine. Hiyo gari ipo tumeisha ipata na ufadhili tumeishapata kutoka *European Union* kwa hiyo huo mpango utaanza wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kupiga zile kura za maoni. Kwenye lile zoezi la kupiga kura za maoni kulikuwa na maelekezo kwamba watu wanaofanya maovu katika jamii watambuliwe, lakini kwa bahati mbaya halikuweka wazi kwamba, wanaowapa watoto wa shule mimba na wanaoendeleza ukeketaji wapigiwe kura.

Mimi naamini kwamba kwenye jamii yoyote, Mangariba wanafahamika, ninaomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine na Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wengine wa dini na Serikali wakitoa ushirikiano wa kuwafichua hao Mangariba wakaripoti, nafikiri watachukuliwa hatua inayokubalika.

Mangariba wako kati yetu na tunawafahamu hatuhitaji kupiga kura ya siri kwa sababu hatuwaogopi naomba wananchi wahamasishwe kuwafichua, na wananchi basi wasiwatumie kwa sababu, usipompeleka mtoto wako kwa Ngariba, hatafanya hiyo kazi, kwa hiyo la muhimu hapa ni kutoa elimu.(*Makofi*)

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linahusiana na mila potofu ambazo zinaleta madhara kwa Wanawake na kwa jamii kwa ujumla.

Je, Serikali imasemaje juu ya mila ya Nyumba Ntobu, hiyo iko *practiced* ambapo bibi mzee ambaye hana watoto huoa binti mdogo halafu wanaume mbalimbali huingia katika nyumba yake ili yule binti aweze kupata watoto, kwa hiyo huwa ni watoto wa baba mbalimbali.

Je, haoni kwamba mila hii inabidi ikatazwe mara moja kwa sababu inasababisha madhara na maradhi mbalimbali kwa Wanawake hao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhonga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mara kulikuwa na hii desturi ambayo sina uhakika kwamba bado inaendelea, lakini tatizo hili lilikuwa linajitokeza kwamba katika mila na desturi za Kiafrika, usipokuwa na mtoto basi wewe huna hadhi ndani ya jamii.

Kwa hiyo, ndiyo ilikuwa inawasukuma akina mama hawa wanakwenda kuoa watoto wadogo, sasa tatizo linakuja ni kwamba sasa basi, anapoendelea kwenda kuzaa na wanaume wengi basi wanakuwa katika hatari ya kupata maradhi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaanzisha vipindi kwenye redio sambamba pamoja na hiki kipindi chetu cha kuondoa ukatili kwa sababu kumuoza mtoto wa kike kwa mwanamke halafu akazaa na wanaume mbalimbali ambao hawapendi mimi naona kwamba ni ukatili.

Kwa hiyo, hii ni sehemu ya ukatili ambayo katika kampeni yetu ya Kanda ya Ziwa tunayoanza sasa hivi basi itakuwa ni sehemu mojawapo ya kupigwa vita kabisa kwa nguvu zote kama tunavyopiga vita ukeketaji, kupigwa kwa Wanawake pamoja na mauaji ya Albino, nafikiri tatizo ndilo hilo.

Basi itakua ni sehemu mojawapo ya kupigwa vita kabisa kwa nguvu zote kama tunavyopiga vita ukeketaji, kupigwa kwa wanawake pamoja na mauaji ya albino.

Mheshimiwa Spika, nafikiri tatizo ndilo hilo ahsante. *(Makofi)*

Na. 14

**Usalama wa Vyombo vya Baharini**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi kavu kuna askari wa barabarani wa kuangalia usalama wa magari:-

(a) Je, Serikali ina mapango gani wa kudhibiti usalama wa vyombo vya majini (Baharini)?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuweka vyombo vya Bahari vya kutoa msaada kwa wavuvi wetu pindi wanapopata matatizo wakiwa majini?

(c) Je, njia gani itumike kwa urahisi katika kuwaokoa wavuvi wanapopata matatizo baharini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) kwa lengo la kudhibiti usalama wa usafiri wa majini na nchi kavu Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Ofisi ya Mrajisi wa Meli ambayo inasimamia udhibiti wa usalama wa vyombo vya baharini.

Vyombo hivi viwili hufanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha ubora wa vyombo vyenyewe, uendeshaji wake kwa msingi kuwa uendeshaji wake wanatakiwa wawe wamepata mafunzo na kuwa na sifa zinazotakiwa pamoja na kuratibu utafutaji na uokoaji katika matukio ya ajali za majini.

Aidha moja ya kazi ya kituo cha mawasiliano cha kuratibu ajari za vyombo vya majini kilichopo Kivukoni Dar es Salaam ni kupata taarifa zenye kuashiria kutokea ajali pamoja na matukio ya ajali zenyewe.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kwa sasa ni kuwa vyombo vyote vinavyofanya shughuli zake baharini huwa na wajibu wa kutoa msaada pale tunapotakiwa kufanya hivyo mara baada ya kupata taarifa kupitia Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji au kuona tukio hilo.

Aidha kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la bahari ni vigumu kwa Serikali kuweka vyombo mahususi kwa ajili ya kutoa msaada kwa wavuvi wanapopata matatizo wakiwa baharini. Pamoja na hivyo matokeo ya ajali yanayoendelea kutoa tishio la vitendo vya uvamizi na uharamia baharini suala la kuundwa kikosi cha Ulinzi wa Pwani yaani *Coast Guard* ili kuimarisha ulinzi, usalama na uokoaji katika maji ya Tanzania ni la muhimu na Serikali italizingatia.

(c)Mheshimiwa Spika, njia rahisi ya kuweza kuwaokoa wavuvi wanapopata matatizo baharini ni kuhakikisha kuwa wakati wote wawapo baharini wanakua na mawasiliano ya kutosha kama vile simu za mikononi, taa za kuashiria tukio la ajali na nyenzo za kujiokolea kama vile *life jackets* ili nyenzo hizo ziweze kuwasaidia wakati wakisubiri kupata msaada wa vyombo vingine vinavyopita karibu au vitakavyokua vimeratibiwa na Kituo cha Utafutaji na Uokoaji hasa ikizingatia kuwa hivi sasa Serikali

imeanzisha Kituo cha Kuratibu Matukio ya Ajili Baharini kilichozinduliwa tarehe 25/3/2009 chini ya Mamlaka ya SUMATRA.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kumwuliza swali moja dogo. Kwa kuwa amekiri kwamba hatuna uwezo mkubwa na pia hakuna *Coast Guard* kubwa.

Kuna mikakati gani ya zaidi ili kuimarisha ulinzi hasa wa *Police Marine* na wale *Navy* ili kuondosha tatizo linalohusu uokoaji na maharamia?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, nikiri tu kwamba tatizo la kuwa na kikosi cha uokoaji kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni la muhimu. Sasa kuimarisha vyombo vingine hivi vya *Police Marine* na vinginevyo ni wajibu wa Serikali kufanya kazi kwa ushirikiano na nataka niahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na vyombo hivi vyote kuhakikisha kwamba suala hili linapewa uzito unastahili.

Lakini niongeze kwamba suala la usafiri wa majini ni pana kwa sababu linategemea mambo mengi lakini kuwepo ujuzi na uzoefu wa uendeshaji lakini vilevile taratibu za upashanaji habari na vilevile kuzingatia ubinadamu kwa vyombo vyenyewe vinavyotoa usafiri kama vile kutokujaza abiria zaidi.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa waendeshaji wa vyombo hivi kuhakikisha kwamba wanazingatia usalama wa vyombo na abiria.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika vyombo vinavyosafiri baharini utaratibu wao wa mawasiliano wana utaratibu wa kupigiana simu za *distance call* na kwa kuwa wavuvi walio wengi wanamiliki simu za mkononi.

Je, ni namba ipi wakiipiga wavuvi itakuwa ni distance call kama ambavyo wanatumia wale ambao wanamawasiliano kwenye vyombo vya baharini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Zubeir Maulid kwa kutoa elimu hii kwamba ziko simu ambazo zinatumika katika kufanya mawasiliano kule baharini hasa ikizingatiwa kwamba yeye mwenyewe ameshawahi kuwa Waziri wa Mawasiliano. Nataka niishukuru sana. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme kwamba kwa haraka haraka kutoa namba ambayo inatakiwa itumiwe naomba tuwasiliane naye ili tukiipata hiyo tuweze kuwapa wote wanaohusika. *(Makofi)*

Na. 15

**Kukarabati na Kupandishwa Hadhi Barabara ya Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Iyogelo –Bugelenga –Nsango –Iponya –Masumbwe –Lugunga –Ushirika –Ivumwa hadi Geita (Bukoli) ina umuhimu mkubwa sana kiuchumi.

(a) Je, kuna hatua gani za kuifanya barabara hiyo iwe ya Mkoa?

(b) Je, ni lini barabara ya Ushirombo (Bukombe) –Buseresere (Geita) ambayo Serikali iliahidi kuitengeneza kwa kiwango kizuri itaanza kutengenezwa japo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupanga barabara katika madaraja unafuata vigezo vilivyowekwa kwenye Sheria mpya ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za Januari mwaka 2009. Barabara ya Iyogelo –Bugelenga –Iponya –Masumbwe –Lugunga –Ushirika – Ivumwa hadi Geita (Bukoli) haikukidhi vigezo vilivyoainishwa kisheria na hivyo haipandishwi daraja kuwa Barabara ya Mkoa.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kutekeleza ahadi ya kujenga barabara ya Ushirombo –Buseresere kwa kiwango cha Changarawe ambayo hivi sasa ni barabara ya Mkoa. Kuanzia mwaka 2005/06 hadi 2008/2009, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Shinyanga imeshatumia jumla ya shilingi milioni 329 kuifanyia ukarabata kwa kiwango cha changarawe pamoja na ujenzi wa daraja la Nyikonge.

Katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitia majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali kwa sasa haina uwezo wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami lakini kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii jitihada za kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe zitaendelea ili barabara hii iweze kupitika wakati wote.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kukiri kwamba barabara ya Ushirombo –Buseresere ni ya Mkoa kwa sababu katika Kikao cha Mkoa huwa wanakataa.

Swali la kwanza kwa kuwa majibu yaliyotolewa katika swali la kwanza la kupandisha hadhi barabara za Masumbe kwenda Bukori Jimbo la Busanda kwenda Geita ninavyoona hayakuzingatia na hawakufuatilia pengine hawakuwa wanaijua barabara waliyoitathimi hiyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akakubaliana na mimi baada ya Bajeti au wakati wowote atakaoona unafaa awatume wataalam wakaiangalie vizuri barabara hii kwa sababu majibu haya yameandikwa mezani?

Swali la pili, kwa kuwa wakati Mheshimiwa Makongoro akiwa Naibu Waziri wa Miundombinu kuna barabara ya Runzewe –Bwanga walikiri kuitengeneza pia kwa kiwango cha lami. Serikali inasema nini juu ya ukarabati wa barabara hiyo na utengenezaji wake.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu vigezo vya kupandisha hadhi barabara hii napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zote zimepitiwa na wataalam na kwa kuwa tulikuwa tunafuata vigezo zilivyokua vimeanishwa Kisheria hivyo vigezo kusema kweli ndivyo viliifanya barabara hii isiweze kukidhi kupandishwa daraja lakini kwa barabara zote tuliunda tume mwezi wa nane mwaka jana kutembelea barabara zote zilizokua zimependekezwa na Mikoa ili ziweze kupandishwa daraja. Lakini pamoja na hivyo nataka nikubaliane naye kwamba licha ya ombi lake la kusema kwamba tutume wataalam mimi mwenyewe nipo tayari kwenda kuitembelea barabara hiyo kwa maana tu ya kutaka kujua jinsi ambavyo tutashirikiana kuitengea fedha kwa ajili ya kuifanyia matengenezo na wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya ambao ndiyo wenye jukumu la kuitengeneza barabara hii.

Swali la pili, kuhusu ahadi ya kuijenga barabara hii. Nasema tutafuatilia ahadi hiyo ambayo ilitolewa na Serikali tuone mazingira ya iliyotolewa na hatimaye tuangalie uwezekano wa kutekeleza ahadi hiyo. *(Makofi)*

Na. 16

**Kima cha Chini cha Mshahara**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitangaza kima cha chini cha mshahara kiwe shilingi 150,000/- na badala yake Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana akatoa kibali watumishi walipwe shilingi 80,000/-.

Je, Serikali haioni kwamba imewachonganisha wafanyakazi na waajiri wao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 100 (2) cha Serikali ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 ana uwezo wa kutoa msamaha katika masuala ya viwango vya ajira *(Employment Standard)* kwa Mwajiri yeyote anayeomba na kuainisha sababu ama mazingira yatakayomfanya ashindwe kutekeleza viwango vilivyowekwa au kukubalika.

Katika zoezi lililofanyika, Waziri baada ya kuona malalamiko ya waajiri walio wengi yangesababisha wafanyakazi wengi kuachishwa kazi na kupoteza ajira zao kutokana na waajiri kushindwa kulipa mishahara kwa sababu ya kupanda kwa kima cha chini cha mshahara alilazimika kutoa misamaha hiyo kwa walioomba ambao wengi ni wale wanaouza zaidi ya asilimia 25 ya bidhaa zao nje kwenye soko lenye ushindani na wale ambao wameajiri zaidi ya wafanyakazi 300.

Lengo ni kulinda uchumi na ajira kwa kumfanya mwajiri asiwaachishe kazi wafanyakazi na wala asifunge kiwanda kwa kuelemewa na gharama za uzalishaji.

Kutokana na malalamiko ya waajiri na wafanyakazi juu ya viwango vipya vya mishahara kuwa mengi siku hadi siku, Serikali alizingatia ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kumtafuta mtaalam mwelekezi (*consultant*). *The Economic Research Bureau, University of Dar es Salaam* kama Mtaalam Mwelekezi, alipewa jukumu la kufanya utafiti wa kina juu na athari zilizojitokeza kufuatia kutangazwa kwa vima vipya vya mishahara katika sekta binafsi. Mtaalam amekwisha wasilisha taarifa ya utafiti na Bodi za Mishahara kisekta zimepitia na kuwasilisha mapendekezo yake kwa Waziri ambaye kwa sasa anazipitia taarifa hizo hatimaye aweze kuziwasilisha katika Baraza la Kazi na Ushauri *(LESCO)* ili nalo limpatie maoni yake kabla hayajatoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kuwa lengo la kutoa msamaha/ kibali cha kulipa mshahara wa shilingi 80,000/- badala ya shilingi 150,000/- ni kulinda uchumi wa nchi na ajira za wafanyakazi na si kuwachonganisha wafanyakazi na waajira wao.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kufahamu kwamba Serikali inakiri kile kitendo cha kuweza kuweka mishahara ya 150,000/- na baadae ikapunguza mpaka 80,000/-. Je, Serikali inakiri kwamba haikufanya utafiti wa kutosha?

Lakini swali la pili napenda kufahamu Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wale waajiri wana uwezo wa kulipa viwango vya juu waweze kulipa tofauti na wanapoweza kutumia hiyo kama *loophole* ya kuweza wote kurudi katika viwango vya chini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, katika kutangaza kima cha chini cha shilingi 150,000/- kwa kweli nia

ya Serikali ilikuwa ni nzuri kabisa na ilikuwa ni kujaribu kuwasaidia waajiriwa na wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwenye maeneo mbalimbali.

Lakini kama nilivyosema baadaye ilionekana kutokana na wadau mbalimbali na hasa wenye viwanda kwamba kulikuwa na hatari ya kuja kupoteza hata kufunga viwanda na kuwaachisha wafanyakazi. Kwa hiyo, kwa sababu Serikali ni sikivu ilibidi isikie na kuangalia kwamba waajiriwa wasifukuzwe na ili viwanda visifungwe kuna haja ya kurudisha chini kile kiwango.

Lakini hata baada ya kurudisha kumekuwepo na malalamiko mengi na ndiyo maana Serikali ikachukua hatua muhimu ya kuteua mtaalam huyu na baada ya muda Serikali itakuwa katika nafasi sasa ya kujua ni vima gani hasa vinastahili kwa maeneo gani na viwanda vya aina gani.

Kuhusu suala la pili, kwamba hawa watatumia mwanya huu kupunguza mshahara wa wafanyakazi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na waajiriwa wote kwa ujumla kwamba kwa kweli katika hatua hii ya pili ambapo tumemtumia mtaalam tunaamin kabisa kwamba vigezo vitakavyokua vinatumika vitakua ni vile ambavyo waajiri hawawezi kupata hiyo *loop hall* ya kupunguza mshahara wa watu kwa sababu itakua imefanyika na wadau wote kwa maana ya Serikali na tunaamini vitakua ni viwango sasa pande zote zitakua zimeridhika.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mshahara wa kima cha chini nchini hupangwa na Serikali. Je ni vigezo gani vinavyotumika katika kupanga mishahara hiyo ili kumwezesha mfanyakazi wa kima cha chini kujitosheleza kwa mahitaji muhimu na ya msingi kwa asilimia 80?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, vigezo vya kuweka viwango vya chini viko vingi lakini kubwa kabisa ni ufanisi au uzalishaji wa kiwanda husika kwa sababu kulipa mishahara itategemea *out put* ya kiwanda au taasisi husika lakini kwa ujumla vilevile tunaangalia uchumi wa Tanzania kwa ujumla wake.

Kwa hiyo, hatuwezi kuweka vigezo ambavyo vitafanya tushindwe kuzalisha kutokana na fedha zote kwa maana ya kushindwa kuendeleza viwanda na taasisi zetu kwa sababu fedha zote zitakua zimeenda kwenye mishahara.

Na. 17

**Maadhimisho ya Siku ya Afya na Usalama Kitaifa**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa siku ya tarehe 28 Aprili ya kila mwaka ni maadhimisho ya siku ya Afya na Usalama mahala pa kazi nchini na Duniani kote, na kwa kuwa maadhimisho hayo huadhimishwa ki-mkoa hapa nchini:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kufanya maadhimisho hayo kitaifa ili wafanyakazi waweze kuifurahia siku hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge Viti Maalum, ningependa kutoa maelezo ya awali kuhusu chimbuko la siku hii ya Afya na Usalama mahala pa kazi Duniani. Tarehe 28 Aprili, 1996 Kamati ya Mji wa New York, Marekani Shirika la Vyama Huru vya Wafanyakazi Duniani kwa kushirikiana na Kaminisheni ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa *(UN-CSD)*, waliwasha mshumaa wa kwanza kabisa kwa ajili ya kuwakumbuka wahanga wa ajali na magonjwa yatokanayo na sehemu za kazi. Kuanzia mwaka huo hadi mwaka 2002 siku hiyo ilikuwa ikiitwa "Siku ya Kimataifa ya Kumbukumbu ya Wafanyakazi waliofariki na walioumia wakiwa kazini. Lengo ni kuwakumbuka wafanyakazi wanaopoteza maisha au kupata ulemavu wa kudumu kutokana na ajali kazini au magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, ilipofika mwaka 2001 Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* lilitambua rasmi siku hiyo na kuziomba nchi zote wanachama wa Shirika hilo zianze kuadhimisha siku hiyo katika utatu (Tripartite) yaani kwa kushirikisha Serikali, waajiri na wafanyakazi. Mwaka 2003 Shirika la Kazi Duniani*(ILO)* lilibadilisha jina la siku hiyo na kuitwa Siku ya Afya na Usalama Duniani." Lengo kubwa ni kwamba pamoja na kuwakumbuka wahanga wa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi iwe pia ni siku ya kuhimiza waajiri, wafanyakazi na jamii kwa ujumla kuboresha mazingira ya kazi. Katika kuadhimisha siku hiyo kunakuwa na shughuli mbalimbali zinazolenga kuhamasisha uboreshaji wa mazingira ya kazi ili kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Tanzania tulianza kuadhimisha siku hiyo rasmi kuanzia mwaka 2004. Katika kipindi hicho siku hiyo imeadhimishwa mara sita hapa nchini katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma. Katika Mikoa yote hiyo siku hiyo ilikuwa ikiadhimishwa katika ngazi ya kitaifa Mikoa yote hiyo ilikuwa ikiadhimishwa katika ngazi ya kitaifa na sio kimkoa kama Mheshimiwa mbunge alivyosema. Shughuli zinazofanyika kwa siku hiyo ni pamoja na maandamano, burudani ya vikundi vya kisanii, kutoa zawadi, salaam za viongozi mbalimbali pamoja na hotuba ya Mgeni Rasmi.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Serikali inazingatia kwa kiasi gani suala zima la tija kwa wafanyakazi kwa maendeleo ya nchi yetu. Je. Serikali itaboresha lini Mahakama za Kazi ili wafanyakazi wasipate usumbufu wa kufuatilia huduma hii mbali kwa kutatua matatizo yao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inazingatia sana swali la tija ya wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi na hili tunalisema kwa sababu hata swali la kwanza nililojibu kuhusu maslahi ya wafanyakazi na mishahara kwa kweli inategemea sana tija.

Kwa hiyo, kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi wafanyakazi wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa tija lakini tunajua vilevile kwamba tija itategemea namna gani maelewano na waajiri yalivyo na namna gani maslahi yao yalivyoboreshwa.

Lakini zaidi ya hapo tunalo Shirika letu la tija ambalo limekuwa likitoa mafunzo mbalimbali namna ya kupandisha tija katika maeneo yetu ya kazi, limekua linafanya semina kwa waajiri na waajiriwa ili kuleta ufanisi na tija kazini. Nipende kusisitiza kwamba Watanzania tuwe na ari ya kufanya kazi kwa tija ili tupandishe uchumi wetu. Lakini vilevile tuboreshe maslahi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mahakama ya Kazi; ni kweli kwamba jambo hili ni muhimu katika kuondoa migogoro maeneo ya kazi na Serikali imelizingatia sana kabla hata ya kufika kwenye Mahakama ya Kazi ambayo sasa hivi yameboreshwa sana. Serikali imeamua kuanzisha Tume ya Kusuluhisha na kutatua migogoro *(CMA)* ambayo imeshaanza na iko chini ya Wizara ya Kazi.

Kwa kweli Tume hii imefanya kazi nzuri sana kwa kipindi hiki kiasi kwamba ni migogoro michache sana ambayo inashindwa kusuluhishwa hadi ifike kwenye Mahakama yenyewe ya Kazi. Tunaamini kwa kuendeleza taasisi hizi tutakua na hali nzuri ya kutatua migogoro maeneo ya kazi ili ufanisi uweze kupatikana.

Na. 18

**Utaratibu wa Uchimbaji Madini Nchini**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (K.n.y. MHE. KAIKA SANING'0 TELELE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Madini inawatambua wachimbaji wadogo wadogo hapa nchini; na kwa kuwa wachimbaji hao mara nyingi ndio waanzishaji wa machimbo ya madini kabla ya machimbo hapo kutambuliwa na Wizara kuwa mgodi na kutoa leseni ya kuchimba madini kwa mwekezaji.

(a) Je, ni halali kwa mwekezaji kuwaondoa wachimbaji wadogo wadogo kwenye machimbo yao kwa maelezo kuwa wakamilishe eneo hilo kwa mujibu wa leseni aliyopewa na madini?

(b) Je, Serikali ina taarifa kuwa mgodi wa Naan katika kijiji cha Engusero – Sambu, Wilayani Ngorongoro umefungwa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa kutokana

mgogoro kati ya Mwekezaji, wanakijiji na wachimbaji wadogo wadogo wapatao 1,700 ambao walikuwa wakijikimu kupitia mgodi huo sasa wameathirika kiuchumi?

(c) Je, ni lini mgodi huo utafunguliwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini husimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na Kanuni zake za mwaka 1999.

Mtu binafsi au kampuni hairuhusiwi kutafuta, kuchimba au kufanya biashara ya madini bila kuwa na leseni ya utafutaji, uchimbaji au biashara ya madini.

Maeneo yanayofahamika kuwa na madini hapa nchini yaligunduliwa baada ya kufanyika shughuli za utafutaji au uchimbaji zilizofanywa na taasisi za Serikali na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na pia wachimbaji wadogo wadogo tangu enzi za ukoloni.

Eneo likishafahamika kuwa na madini na mashapo ya madini ya kutosha kuchimbwa kwa faida, mgodi huanzishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Bwana Jumbe Rajabu Kunga na wenzake wanne walipewa leseni mbili za uchimbaji mdogo wa madini *(Primary Mining Licence) PML 0010810* na *PML 0010811* kwa ajili ya kuchimba madini ya vito aina ya spessartite katika eneo la Kijiji cha Engesero Sambu, Wilaya Ngorongoro.

Ni utaratibu wa kawaida kwamba baada ya leseni kutolewa kwa mujibu wa kifungu Na. 95 cha Sheria ya madini ya mwaka 1998 mwenye leseni baada ya kulipa fidia endapo eneo husika linamilikiwa na mamlaka yoyote kama kijiji au hifadhi.

Bwana Jumbe Rajabu Kunga na wenzake waliingia mkataba na Serikali ya kijiji cha Engusero –Sambu, tarehe 29 Aprili, 2008 ili kuweza kuchimba madini ya vito katika maeneo ya leseni zilizotolewa kwa Bwana Jumbe Rajabu Kunga na wenzake.

Bodi ya pamoja baina ya Bwana Jumbe Rajabu Kunga na wenzake wanne za Serikali ya Kijiji ina jukumu la kupanga na kuratibu shughuli za uchimbaji wenye tija kwenye mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini hairuhusu kupandanisha leseni kwenye eneo moja. Katika eneo la leseni za Bwana Jumbe Rajabu Kunga na wenzake hakukuwa na leseni yoyote ya uchimbaji mdogo hivyo wachimbaji katika eneo hilo walikuwa wanachimba kinyume cha sheria.

(b)Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inazo taarifa za kusitishwa, kwa muda kwa shughuli za uchimbaji katika mgodi wa Naan katika kijiji cha Engusero –Sambu. Shughuli za uchimbaji katika mgodi wa Naan zilisitishwa na Katibu Tarafa wa Loliondo kwa barua ya tarehe 8 Julai, 2008 kutokana na kuwepo wachimbaji wasio na leseni katika eneo lenye leseni ya watu wengine.

Aidha, uchimbaji huo ulikuwa hauzingatii kanuni za usalama wa mazingira na pia madini yaliyochimbwa yalielekezwa kwenye mkondo haramu kwa kusafirishwa kwenda nchi jirani.

(c) Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 24 Aprili, 2009 Wizara yangu kupitia Ofisi ya Madini Arusha iliwaelekeza wenye mgodi Jumbe Rajabu Kunga na wenzake kwamba mgodi wao ulipaswa kuanza kazi kuanzia tarehe 1 Mei, 2009.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inapotoa leseni kwa kampuni au kwa mtu mmoja mmoja na kuwapa eneo ambalo wananchi wamekwishachimba; na kwa kuwa umaskini umekuwa mkubwa sana nchini kwa hiyo wananchi wanatafuta kila njia ya kutafuta kipato au kujiajiri; je Serikali inapompa mwekezaji eneo hilo ambalo wananchi wanajitafutia, wanahemea pale, haioni kwamba inasababisha vurugu na ndio maana wananchi wanachukua hatua ya kuvunja sheria na kuchukua sheria mkononi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba, wawekezaji tunaowaongelea ni pamoja na wawekezaji wa ndani siyo wawekezaji wa nje tu, lakini ni suala la kiutaratibu.

Mheshimiwa Spika, itakuwa vurugu endapo tutaruhusu shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini zifanyike bila kufuata taratibu, kwa ajili ya kurahisisha uratibu na usimamizi kwa maslahi ya pande zote mbili. Kikubwa ni kwamba, kama Serikali, tunaendelea kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kama ambavyo mara kadhaa tumeshatoa ufafanuzi kupitia Bunge lako Tukufu, lakini pia matamko mbalimbali ya Serikali. Utaratibu huu utatusaidia sana, kwa sababu utawajengea mazingira mazuri zaidi na pia kuwaandalia utaratibu mzuri wa kuwawezesha kwa ajili ya kuboresha shughuli zao na hasa ndugu zetu wachimbaji wadogo.

**MHE. JOHN SAMWEL MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa knipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Busanda kuna watu wengi sana ambao wangependa kuingia katika uchimbaji mdogo mdogo wa dhahabu na sehemu ile imejaliwa kuwa na sehemu nyingi sana zenye dhahabu lakini tatizo lao kubwa ni kupata maeneo ambayo

wanaweza kupewa kisheria. Je, Waziri anawaahidi nini watu wa Busanda ambao wanapenda kuwa na sehemu za uchimbaji mdogo mdogo wa dhahabu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Jimbo la Busanda lililoko Wilayani Geita ni kati ya maeneo ambayo yamebarikiwa sana katika nchi yetu kuwa na rasilimali ya madini mengi. Nipende tu kulihakikishia Taifa kwa mara nyingine tena kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, Wilaya ya Geita na hasa Jimbo la Busanda ni kati ya maeneo ambayo pia yameshafanikiwa kwa kiwango kikubwa, kwa sasa hivi kufaidika na usimamizi na uratibu mzuri wa Serikali kuhusu mkakati wa kuwawezesha wachimbaji wadogo, kwa maana ya kwamba, eneo la Rwamgasa ambalo ni mojawapo ya Kata 13 za Jimbo la Busanda, tayari tumeshatenga hekta 710 ambazo tayari zilishatolewa leseni kwa wachimbaji wadogo kuanzia mwanzoni mwa mwaka huu. Si hivyo tu, eneo la Nyarugusu ambalo pia ni miongoni mwa Kata hizo 13 za Jimbo la Busanda, tumeshatenga na kugawa leseni kwenye maeneo ya hekta 510.

Mheshimiwa Spika, bado tunaendelea kuyafanyia utaratibu maeneo mengine ambayo tunahisi kwamba, pengine hayafai sana kwa wachimbaji wakubwa, lakini yanaweza kuwa na rasilimali ya kutosha kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoendelea kuwaahidi Wananchi wa Busanda kupitia Mbunge wao, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba ni kwamba, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha wachimbaji wadogo na hasa kwa utaratibu tunaokuja nao wa Mfuko wa kuwawezesha wachimbaji wadogo waendelee kunufaika, mradi ambao tunaamini kwamba utakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali umepita kidogo, lakini tuna swali moja tu, ningeomba tulimalize hilo. Nimetaarifiwa kwamba, swali hili ambalo ni la Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

Na. 19

**Kupeleka Umeme Vijijini**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA (K.n.y. MHE. TATU MUSSA NTIMIZI)** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kupeleka umeme vijijini *(Rural Electrification)* ni moja ya ahadi za Serikali iliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; na kwa kuwa mwaka 2007 wataalamu kutoka Tabora walipita kwenye Jimbo la Igalula kuona maeneo na kuwapa wananchi matumani kuwa huenda mchakato wa kuweka umeme Jimboni humo umekaribia kuanza:-

(a) Je, ziara hiyo inatupa taarifa gani ya matumaini ya kupata umeme kwenye Jimbo hilo?

(b) Kwa kuwa mwezi Oktoba/Novemba, 2008 Mheshimiwa Rais alitembelea Kijiji cha Kigwa kilichopo Jimboni Igalula na moja kati ya maombi ya Mwenyekiti wa Kijiji kwa Mheshimiwa Rais ni kuona uwezekano wa kuvuta umeme kutoka Tabora Mjini hadi Kigwa (umbali wa kilomita 50). Je, Serikali inalifahamu suala hilo na kama inalifahamu, inawaambia nini Wananchi wa Kigwa na Jimbo la Igalula juu ya uwezekano huo na lini mradi utaanza?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, ambalo limeulizwa kwa niaba yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitoe maneno ya utangulizi kabla ya sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Ntimizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli suala la kupeleka umeme vijijini ni moja ya ahadi za Serikali iliyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 na hasa katika ibara ya 90. Serikali inajitahidi kufanya usambazaji wa kupeleka umeme vijijini kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, tatizo ama changamoto inayotukabili ni kuhusu upatikanaji wa rasilimali fedha kwa wakati na kuhusu miradi ambayo tumeiainisha ili itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, bada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ziara zinazofanywa na Wataalamu wa TANESCO kama hiyo iliyofanywa katika Jimbo la Igalula ni utaratibu wa kawaida wa Shirika wa kutembelea na kukagua maeneo yenye kuhitaji huduma ya umeme katika maeneo yao na katika Mkoa wa Tabora. Ziara hizi huwezesha kupata makadirio ya gharama za kupeleka umeme na idadi ya wateja watarajiwa. Gharama hizi huwekwa kwenye mipango ya utekelezaji, ambayo hutegemea upatikanaji wa fedha. Ziara hizi hufanywa kila mwaka kutegemeana na bajeti za kazi zilizopo ili kupata takwimu halisi kwa wakati unaohusika. Makadirio ya gharama husika za utekelezaji wa mradi zinaendana na wakati ambao mradi unakuwa unatekelezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Kigwa na baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa tathmini katika Jimbo la Igalula, kwa ujumla unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi 4,268,897,265. Mradi huu utajumuisha ujenzi wa kilomita 85 kwa ujumla ukijumuisha na zile ambazo Mheshimiwa Mbunge ameulizia za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutoka Tabora Mjini, ufungaji wa transfoma 16 na ujenzi wa kilomita 21 za njia ya umeme msongo wa voti 400. Maeneo na vijiji vitakavyofaidika ni pamoja na Idala, Kinamagi, Kigwa B, Igalula, Imalaseko na Goweko.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwataarifu Wananchi wa Jimbo la Igalula kwamba, Serikali iko makini na suala hili na inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha kwamba, mradi huo unatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa matatizo ya Wananchi wa Jimbo la Igalula yanafanana kabisa na matatizo ya Wananchi wa Jimbo la Karagwe; na kwa kuwa Serikali tayari ilishapima maeneo ya kupeleka umeme katika Jimbo la Karagwe kuanzia Kayanga – Rwambaizi, Bugene – Kiluluma – Nyakaiga, Bugene – Nyaishozi – Yembe; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi kwa muda mrefu kupeleka umeme katika vijiji hivyo na sasa hivi tunakaribia mwisho wa mwaka wa fedha; je, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini Wananchi wa Jimbo la Karagwe wa vijiji hivyo na kwamba umeme utakwenda lini kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nikianzia na sentesi ya mwisho ya swali la nyongeza, isingekuwa angalizo ambalo nilipewa mwaka jana na Mheshimiwa Mtutura. Ningesema tu kwamba, Mheshimiwa Blandes kwa niaba ya Wananchi wa Karagwe, vuteni subira kwa sababu mipango ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Jimbo la Karagwe ipo.

Mheshimiwa Spika, kikubwa naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Karagwe kwamba, tuna mipango ambayo tumeshaiandaa na nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane kwenye ofisi yetu. Yapo mambo mengi ningependa kuyasema, lakini kwa sababu tuko kwenye kipindi cha bajeti, taarifa nyingi zitajitokeza wakati wa mawasilisho ya hotuba ya makadirio yetu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya umeme kwa mwaka unaokuja wa fedha wa 2009/2010. Naamini kwamba, Mheshimiwa Blandes na Wananchi wa Karagwe watafarijika. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la mwisho.

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kusaidia kuondoa tatizo la umeme Mjini Songea na kwa ahadi ya Serikali ni kwamba mwezi huu umeme katika Mji wa Songea utakuwa hauna tatizo; na kwa kuwa kuondokana kwa tatizo la umeme katika Mji wa Songea kutasaidia umeme kuwashwa katika Mji wa Peramiho, eneo ambalo sasa hivi TANESCO wanaendelea kufanya *installation* ya nguzo za umeme kwenda kule Peramiho; je, Mheshimiwa Waziri anataka kunihakikishia leo kwamba haya mambo yote mawili yataendana kwa pamoja na hivyo basi haraka sana mwezi wa saba umeme utawaka pia katika Mji wa Peramiho kama vile Mji wa Songea?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli napenda kutumia nafasi hii kumhakikishia yeye Mheshimiwa Mbunge kama nilivyomhakikishia jana wakati tulipokuwa na mazungumzo ya siri yeye na mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasema ya siri kwa sababu yalikuwa nje ya ukumbi huu. Lakini ni kweli kabisa kwamba, tutakapokuwa tunakamilisha na tunatarajia mwishoni

mwa mwezi huu kukamilisha ufungaji wa jenereta mpya katika Mji wa Songea, itaturahisishia sasa kukamilisha ujenzi wa miundombinu na kuwasha umeme katika eneo la Mji wa Peramiho na maeneo mengine ambayo yanapitiwa na njia hiyo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kutueleza kwamba, kuna uwezekano pia wa mazungumzo ya siri katika masuala haya. Sina hakika yanahusu jinsia zote!

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo; nikianza na wageni, kwa heshima naomba nimtambulishe kwenu Mheshimiwa Balozi Nguyen Du Stuen, ambaye ni Balozi wa Vietnam hapa Tanzania, yuko pale *Speaker's Gallery*. *(Makofi)*

*Your Excellency, we are very honoured to have you with us here. Our relationship with the Vietnam over the years has been very warm and we are continuing to learn from your success in the agricultural sector. Thank you for being here in Dodoma. (Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, ambao ni Ndugu Asha Omar – Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Kigoma; naomba asimame tumtambue. Yule pale! Ndugu Pili Mvunye – Katibu wa UWT, Mwandiga, Kigoma. Ahsante sana. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Maria Hewa ambao ni Ndugu Maimuna Yussuf – Mwenyekiti wa UWT Kata ya Nyakato, Mwanza, Ndugu Salima Mchele – Katibu wa CCM Kata ya Nyakato na Ndugu Witness Makale – Mkereketwa tu wa CCM. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe. Aaah! ni mgeni mmoja tu anaitwa Nyawili Kalenda. Yupo? Yule pale. Sifa yake ni kwamba, yeye ni Mchambuzi Mkakati Maalumu wa Jimbo la Songwe. Mambo yanakwenda kisayansi kweli, hongera sana. *(Kicheko)*

Ndugu Lilian Mwinula naye tunaye hapa ni Meneja wa Kanda ya Kati wa Benki yetu ya NMB. Lilian Mwinula, naona hayupo!

Wapo pia wanafunzi 85 na Walimu 5 kutoka Southern Highland School Mafinga. Sijui ni kweli? Ndio wale kule, ahsante sana. Hii ni shule maarufu sana. Tunawakaribisha sana hapa na kwa vijana tunawatakia mafunzo mema na Walimu tunawatakia kazi njema.

Vikao: Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa idhini maalumu ya Mheshimiwa Spika, ameruhusiwa kufanya mkutano saa 5.00 asubuhi kwa sababu mikutano yote hii ya Kamati sasa itakuwa ni baada ya saa 7.00 ili kukamilisha hoja za bajeti za sekta hii. Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, saa 5.00 asubuhi hii, Ukumbi Namba 210, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 227.

Natangaza kwamba saa 4.30, Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, tukutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa hadi saa 5.30 na baada ya hapo ndiyo tutakuwa na kikao na Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri aliowateua ili kuzingatia masuala ya bajeti. Kwa hiyo, saa 4.30 hadi saa 5.30, halafu saa 5.30 na kuendelea awamu ya pili ya kikao hicho. Naomba Wenyeviti wa Kamati za Kudumu wote mhudhurie kikao hicho muhimu. Kutokana na tangazo hilo basi, nalazimika kuondoka kwenye Kiti na namwomba Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, aje hapa ili kuendeleza shughuli zilizosalia za asubuhi hii. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009
***(The Executive Agencies (Amendment) Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009 *(The Executive Agencies Amendment Bill, 2009),* sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wakati Kamati ilipokutana Mjini Dodoma jana tarehe 9 Juni, 2009. Ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote, waliotoa michango yao wakati wakichangia marekebisho ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tumezingatia michango ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na tumekwishaifanyia kazi kama inavyoonekana kwenye kiambatisho cha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Mweyekiti, Sheria ya Wakala wa Serikali inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho, ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 31 Oktoba, 1997 na utekelezaji wake ulianza tarehe 12 Desemba, 1997. Sheria hii ilitungwa mahususi ili kuweka utaratibu wa uanzishwaji na uendelezaji wa Wakala wa

Serikali, ambao pamoja na malengo mengine, huanzishwa ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma kwa jamii katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, sasa ni takriban miaka 11 tangu Sheria hii ilipoanza kutumika. Katika kipindi hicho, mabadiliko mbalimbali yametokea ikiwa ni pamoja na mabadiliko katika Sheria nyingine ambazo zinagusa utendaji wa Wakala. Marekebisho yanayopendekezwa yanatarajiwa kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii na kuongeza ufanisi katika shughuli za Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu: Sehemu ya kwanza, inaeleza mambo ya awali ya Muswada kama vile Jina la Sheria. Sehemu ya pili inahusu mapendekezo ya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheia ya Wakala wa Serikali. Sehemu ya tatu inaonesha Sheria zitakazobadilishwa ili ziende sambamba na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya pili ya Muswada huu, inapendekezwa kufanyia marekebisho kifungu cha pili cha Sheria ya Wakala wa Serikali ili kutoa tafsiri ya *Appropriate Authority*, kumaanisha idhini kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi ya kuanzisha Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia unapendekeza kufanya marekebisho ya kiuandishi katika vifungu namba tatu na namba nne vya Sheria hii, kutoa maana iliyokusudiwa katika mafungu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tano cha Muswada huu, inapendekezwa kirekebishwe ili kubainisha mipaka ya kimamlaka ya Makatibu Wakuu, juu ya uendeshaji wa Wakala wa Serikali. Marekebisho haya yanakusudia kuwapa Makatibu Wakuu jukumu la kusimamia na kutoa miongozo kwa Wakala wa Serikali katika masuala ya kisera tu, tofauti na ilivyo sasa ambapo mamlaka ya Makatibu Wakuu juu ya Wakala wa Serikali ni makubwa mno kiasi cha kuweza kusababisha matumizi mabaya ya mamlaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa pia katika Ibara ya sita ya Muswada huu kufanya marekebisho katika kifungu cha sita cha Sheria ya Wakala wa Serikali ili kuwaondoa Makatibu Wakuu kwenye nyadhifa za Uenyekiti na Ujumbe wa Bodi wa Ushauri wa Wakala wa Serikali, kwa lengo la kwenda sambamba na misingi ya Utawala Bora. Ibara hii pia inapendekeza kuwazuia Watendaji Wakuu Serikalini na Wanasiasa kuwa Wajumbe wa Bodi za Ushauri za Wakala wa Serikali kwa dhamira hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha saba cha Muswada huu kinapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha saba cha Sheria ya Wakala wa Serikali. Pia katika kifungu hiki, inapendekezwa kupanua wigo wa maeneo ambayo Bodi ya Ushauri wa Wakala wa Serikali inaweza kuyatolea ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya nane ya Muswada huu inapendekeza kufuta na kupendekeza kifungu kipya cha tisa cha Sheria ya Wakala wa Serikali ili kuifanya Sheria

hii iende sambamba na marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2007, yaliyoanzisha Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara tisa ya Muswada huu inapendekeza kuongeza kifungu cha 10 kwa madhumuni ya kuboresha ibara hiyo ili iweze kusomeka vizuri, pamoja na kumaanisha kazi za Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10 kinapendekeza marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali ili kutoa nafasi ya kukata rufaa kwa Tume ya Utumishi wa Umma, kwa mtumishi yeyote wa Wakala wa Serikali dhidi ya maamuzi ya Mtendaji Mkuu. Aidha, kwa mtumishi ambaye hataridhika na maamuzi ya Tume ya Utumishi wa Umma chini ya marekebisho yanayopendekezwa, atakata rufaa kwa Rais kupitia kwa Katibu Mkuu Kiongozi, kama ilivyo kwa watumishi wote wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa katika ibara ya 11 ya Muswada kufanya marekebisho katika kifungu cha 13 cha Sheria ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato vya Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 12 ya Muswada inafanya marekebisho ya kiuandishi katika fungu la 18 la Sheria ya Wakala wa Serikali ili kutoa maana halisi inayokusudiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara za 13, 14, 15 na 16, zinapendekeza marekebisho katika baadhi ya Sheria ili kuweza kufanya marekebisho yanayofanana na yaliyopendekezwa katika Sheria ya Wakala wa Serikali. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma, Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na baadae nitaomba Bunge lako Tukufu liweze kupitisha ili hatimaye kwa kadiri itakavyokuwa, Mheshimiwa Rais aweze kutia saini na uwe Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili naye atoe mchango wake hapa. Mpaka sasa tunalo jina moja tu la aliyeomba kuchangia Muswada huu.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la

mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ilitekeleza kazi ya kuujadili Muswada huu tarehe 9 Juni, 2009 katika Ofisi ya Bunge Dodoma na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu marekebisho yaliyokusudiwa ambayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, imeridhika na maudhui na madhumuni ya Muswada huu ambao una lengo la kurekebisha upungufu uliomo katika Sheria ya Wakala wa Serikali, sura ya 245, ili iweze kutekelezwa katika mfumo mzuri zaidi wa kuimarisha utendaji na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umefafanua vizuri, utata wa siku nyingi ambao ulikuwa hauoneshi mipaka ya Katibu Mkuu katika uendeshaji wa Wakala za Serikali, zilizokuwa chini ya Wizara zao na wakati mwingine Makatibu hao hutumia vibaya mamlaka yao. Suala hili sasa limefafanuliwa vizuri katika kifungu cha tano cha Muswada huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo katika vifungu vya Muswada:-

(a) Kifungu cha 15(4) kinachoongelea nafasi za viongozi wa kisiasa, Kamati inapendekeza kuwa itolewe maana ya neno "*political post*" ili ieleweke wazi ni viongozi gani wa kisiasa wanaokusudiwa.

(b) Katika kifungu cha 10 Kamati inapendekeza kuwa, Rais asiwemo katika mfumo wa rufaa kutokana na majukumu mengi aliyonayo. Kamati inapendekeza rufaa hizo ziishie kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

(c) Kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato, Kamati inakubaliana na pendekezo la Muswada la kupeleka Hazina mapato yote yanayokusanywa na baadae kugawiwa wakala mbalimbali ambazo hapo awali zilitegemea ruzuku ya Serikali. Lengo ni kufanya mgawanyo uwe sawa na kuondokana na kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha maoni hayo machache, kama nilivyosema awali, kwa ujumla Kamati yangu imeridhika na mapendekezo yaliyokusidiwa katika Muswada huu, ambao Kamati inaamini kuwa utasaidia sana kuimarisha Utawala Bora na vilevile kwenda na wakati kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii, kwa kutoa mchango wao wa kina wakati wa kujadili Muswada huu. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za kisiasa na kijamii, ndio umefanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Juma Omar, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru, Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa, bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Ramadhan Abdallah na Ndugu Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati, sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa suala hili.

**MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni kuhusu marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Wakala wa Serikali ya Mwaka 2009 *(The Executive Agencies (Amendment) Act, 2009).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na hivi sasa niko mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Wakala wa Serikali ya Mwaka 2009 *(The Executive Agencies (Amendment) Act, 2009)*, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa ujumla haina tatizo wa kupingana na dhana nzima ya Muswada, japokuwa kuna angalizo tunalotaka Mheshimiwa Waziri alitafutie ufumbuzi ili kuondoa uwezekano wa kuwepo na malalamiko ya hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kutambua jinsi ambavyo hazina imeonesha mfano kwa asasi zile ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha, ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa

Hesabu za Serikali, kuhusu kuondolewa kwa viongozi wenye nyadhifa za kisiasa kuwa Wenyeviti au Wajumbe wa Bodi katika Taasisi za Umma. Aidha, kuwaondoa Makatibu Wakuu wa Wizara kwenye nafasi za Uenyekiti wa Bodi zilizo chini ya Wizara husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, watu wote wenye nyazifa za kisiasa wasiteuliwe kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Hii ni kuunga mkono mapendekezo ya *CAG* nanukuu: "Ili kuboresha Utawala Bora, Wabunge wasiteuliwe kwenye Bodi za Mashirika ya Umma. Aidha ni pamoja na kutekeleza pendekezo la *CAG* na maazimio ya mkutano wa uwajibikaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. *(Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi na nitachangia kwa ufupi sana, Muswada huu ambao uko mbele yetu, ambao umewasilishwa na Waziri anayehusika na Utumishi kuhusu mabadiliko ya Sheria za Wakala wa Serikali. Nina hoja ya kwanza inayohusiana na mabadiliko ambayo Waziri ameyaleta ya kuwaondoa watu wote wenye nyadhifa za kisiasa kwenye Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya pili mfululizo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amekuwa akitoa pendekezo hili kuhakikisha kwamba, tunatofautisha majukumu yetu kama Wabunge na Wanasiasa wengine ya kusimamia majukumu ya utendaji wa kila siku, ambazo Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika mbalimbali zinafanya.

Muswada huu unawaondoa wanasiasa kwenye Bodi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo NSSF, PSPF na LAPF. Hivi karibuni Gavana wa Benki Kuu, ametoa agizo maalumu kwa vyombo vyote vya kifedha na kwamba Wabunge, Madiwani na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, hawaruhusiwi kuwa Wajumbe wa Bodi katika vyombo vyote vya kifedha.

Lengo letu ni kuona kwamba, maamuzi ya CAG yanatekelezwa katika hali ambayo ni ya asilimia mia moja. Kwa hiyo, tungependekeza na mezani kuna *schedule of amendments* ya kutaka sehemu fulani fulani za Sheria ya Mashirika ya Umma zifanyiwe marekebisho ili kuhakikisha kwamba, tunatekeleza agizo hili la mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara moja kwa kuwaondoa Wanasiasa na Watendaji wa Serikali. Ninaomba nisisitize kwamba, suala sio kuwaondoa wanasiasa tu, bali pia Watendaji wa Serikali kwa maana ya Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali, ambao wengine ni Wajumbe wa Bodi au ni Wenyeviti wa Bodi mbalimbali za Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, suala hili nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri alikubali kwa sababu utakuwa ni utekelezaji na kuimarisha Utawala Bora kama ambavyo wameanza na hatua hizi. Hatuoni sababu ni kwa nini wanasiasa waondolewe kwenye Bodi za Wakurugenzi

wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii, waachwe kwenye Bodi nyingine ambazo majukumu ni yale yale .

Pili, kuna suala zima la Wakala hizi kutakiwa kutoa fedha zake kwenda Hazina. Tunafahamu kabisa hivi sasa Serikali lazima ihakikishe ya kwamba, inadhibiti vyanzo vyake vyote vya mapato ili tuweze kupata mapato na kuweza kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo, lakini tunapokuwa tunachukua fedha kutoka kwenye Wakala hizi, lazima tuzingatie majukumu ya kiutendaji ya zile Wakala.

Tukichukua fedha bila utaratibu maalumu na bila kufuata hali ambayo itapelekea bajeti ya zile Wakala ziweze kutekelezwa vizuri, tutajikuta tunaziua na kuondoa maana halisi ya hizi Wakala. Kwa hiyo, hili pia nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kuliangalia ili kuhakikisha fedha za Wakala zinatumika katika shughuli ambazo zimewafanya waweze kuundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu katika Muswada huu ni hayo tu na tunaisubiri Kamati ya Bunge Zima ili tuweze kuleta hizo *Ammendments* ambazo zinatakiwa. Nakushukuru sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge na yamehitaji ufafanuzi. Kabla ya kutoa ufafanuzi, ningependa kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika uchaguzi ambao ulikuwa na vishindo vya aina yake kule Busanda. Hongera sana kwa kutuongezea idadi ya akina mama Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ningependa nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa maelekezo na ushauri wao ambao walitupatia tukiwa kwenye Kamati.

Ningependa kuchukua nafasi hii, kumshukuru Bwana George Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Bwana Erick Shitindi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa msaada wao mkubwa ambao umeniwezesha kuwasilisha Muswada huu Bungeni na sasa hivi kuweza kuutolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda sasa niwatambue wale ambao wamechangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwa mchango aliouwasilisha kwa niaba ya Kamati. Pia ningependa kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa maoni ambayo yote yalikuwa na lengo la kuuboresha Muswada wetu.

Ningependa kuchukua nafasi hii, kumtambua Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa mchango wake. Pia nimshukuru Mheshimiwa Pindi Chana, kwa mchango wake wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ningependa sasa nianze kujibu hoja ambazo zimetolewa na wachangiaji ambao wamechangia katika Muswada wetu.

Suala la kwanza ambalo Kamati ingependa litolewe ufafanuzi au tulijibu ni la kutoa tafsiri wa Viongozi wa Kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, marekebisho mengi ambayo tulipewa jana na Kamati, tuliyafanyia kazi na yapo katika *schedule* yetu ya *amendment.* Sasa kwa tafsiri nyepesi tu, Viongozi wa Kisiasa ni kama sisi Wabunge, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na kama ambavyo imetafsiriwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeulizwa ni ambalo Kamati imeomba tulifanyie kazi; Kamati imependekeza kwamba, Rais asiwe katika mfumo wa rufaa kutokana na majukumu mengi aliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilipenda nitoe taarifa kwamba, kwa sheria tulizonazo sasa hivi, Watumishi wote wa Umma baada ya kuwa wamepeleka malalamiko yao katika Kamati mbalimbali na kupelekwa katika Tume ya Utumishi wa Umma kama rufaa, Mtumishi yeyote asiporidhika, anakata rufaa kwa Mheshimiwa Rais isipokuwa Watumishi wa Wakala wa Serikali tu.

Sasa tumeona ni busara nao tukawapa uwigo mpana, pale ambapo hawaridhiki na maamuzi ambayo yametolewa, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Serikali isiwe mwisho na yeye apate fursa sawa na zile ambazo wanazipata watumishi wengine wa Umma wa kukata rufaa kwenye Tume ya Utumishi wa Umma na wasiporidhika basi waweze kwenda mbele zaidi hata kwa Mheshimiwa Rais.

Mara nyingi rufaa zinazokwenda kwa Mheshimiwa Rais ni chache sana, kwa hiyo, ningependa niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mheshimiwa Rais ana majukumu mengi sana, asipelekewe hizi rufaa kwa kufikiria labda ziko nyingi mno kiasi kwamba hawezi kuzishughulikia .

Mara nyingi rufaa zinazoenda kule ni chache sana, nyingi zinaishia katika Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa na ambalo limetolewa na Mheshimiwa Zitto, anapendekeza kwamba kupitia Bunge hili tuwaondoe Wabunge wote kwenye Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Zitto kwamba, Muswada uliopo mbele yenu ni wa Marekebisho ya Wakala wa Serikali na lengo lake kuu ni kuwaondoa Makatibu Wakuu kwenye Wakala za Serikali, ambazo ziko chini ya Wizara zao; kama nilivyosema katika masuala mazima ya kuwa na utawala bora na tulivyozungumzia mifuko ya *pension* yote ile, ukichukulia Mfuko wa LAPF, Mwenyekiti wake alikuwa ni Katibu Mkuu wa TAMISEMI; ukienda Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma, Mwenyekiti wake alikuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, katika kuwa na Utawala Bora na ili kuwapunguzia wasijichukulie madaraka makubwa katika Mifuko hiyo na katika hizi Wakala za Serikali, ndio maana tukaleta sheria hii ili kuwaondoa Makatibu Wakuu. Sambamba na hilo, kwa sababu tunairekebisha Sheria ya Wakala wa Serikali, tukasema kwenye hii Sheria si Makatibu Wakuu tu, bali hata na wanasiasa pia tunawaondoa wasiwe Wajumbe katika Wakala hizi; hii yote ni katika kusisitiza Utawala Bora.

Suala lingine ambalo Mheshimiwa Zitto amelisema ni suala zima la kwamba, kwa nini waondolewe wanasiasa tu na si Makatibu Wakuu. Nadhani nimekwishalijibu kwamba, kwenye Wakala za Serikali, Makatibu Wakuu tumewaondoa na ndio lilikuwa lengo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, masuala ambayo yamenifikia mezani kwangu ndio hayo na ambayo nimeyatolea hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009
### *(The Executive Agencies (Amendment) Bill, 2009)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16 kama *Schedule of Amendment* inavyoonesha, napendekeza kiongezwe kifungu cha 17. Kabla ya hapo, maelezo ambayo ningependa kuyatoa, yanatokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza kuhusiana na mabadiliko ya Sheria hii na kwamba, hoja niliyoitoa iko nje ya Muswada.

Napenda nimrekebishe Mheshimiwa Waziri kwamba, *Part Three* ya Muswada ni *consequential amendment.* Tunabadilisha Sheria nyingine mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kama mwenyewe alivyosema, *likely* baadhi ya *Pension Funds,* Wenyeviti wao walikuwa Makatibu Wakuu.

Napenda nimkumbushe tu kwamba, moja ya *Pension Fund* ambayo inafanyiwa marekebisho ni NSSF, ambayo haipo kisheria. Mwenyekiti wake atakuwa ni Katibu Mkuu na hata huyu ambaye sasa ni Katibu Mkuu, alikuwa Mwenyekiti kabla hajawa Katibu Mkuu. Kwa hiyo, haiendani kabisa na hoja ambayo alikuwa ameizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ambayo ninaileta ni kwamba, tuongeze kifungu cha 17 mara baada ya kifungu cha 16 kwenye *consequential amendments* kwamba; *The Chairman and Members of the Board shall not be persons holding any political post or being Chief Executives of the Government* na hapa tunafanya *amendment* ya *Public Corporations Act, 1992.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *Amendment* sisi hatujaipata, inavyoonesha haikuja kwa wakati; haijafika ofisini kwetu wala kwa AG.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Amendment* zinakwenda kwa Katibu wa Bunge na ndiye mwenye jukumu, haziendi mezani kwa Waziri. *Amendment* inakwenda kwenye meza ya Bunge na imefuata taratibu zote, nimepita katika Idara ya Sheria ya Bunge, nilikokuwa naomba Bunge likubaliane na *Amendment* hiyo ili kuweza kuhakikisha kwamba, tunaimarisha Utawala Ubora katika Taifa letu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwarejeshe kwenye Kanuni ya 88 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambayo inaeleza yafuatayo:-

Ukisoma ile ya pili inasema; mabadiliko yote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria, sharti yawekwe katika jedwali la mabadiliko litakaloandaliwa kwa ajili hiyo na kugawiwa kwa Wabunge katika kujadili na ama kuyapitisha au kutoyapitisha vyovyote itakavyokuwa. Sasa kama tunavyosema, haya mabadiliko hayajaletwa kwetu wala hayajawasilishwa kwa Wabunge, kwa hiyo, kanuni hii haijazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa ombi kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Hawa Ghasia, sisi hatuna hayo marekebisho kwa hiyo hatuyatambui.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kaa kwanza. Inaelekea umechelewa kuyawasilisha mabadiliko yako.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhaali; moja ya jukumu lako hapo mezani ni kutenda haki.

**MWENYEKITI:** Usini-j*udge* wewe zungumzia *issue* yako.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Nimefuata taratibu zote, sio jukumu la Mbunge kugawa marekebisho. Nimeyaleta mezani kwa taratibu zote kwa mujibu wa kanuni; kama Serikali haijapata hiyo ni shida ya Serikali, kwa sababu marekebisho yamekuja na taratibu za Bunge zifanyike. Sasa kama watu hawajatekeleza wajibu wao ni wao, mimi nimetekeleza wajibu wangu na ninaomba Bunge likubaliane na marekebisho hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, taarifa tuliyonayo mezani ni kwamba, mabadiliko yamefika robo saa tu iliyopita. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni inasemaje kuhusu marekebisho; yanakuja kwa muda gani; marekebisho yamepelekwa kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge toka saa tatu asubuhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nalazimika ku-*rule out* badiliko lako ili tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima taratibu za Bunge zifuatwe; Mbunge amefuata taratibu zote zinazotakiwa, suala la ugawaji wa mabadiliko sio suala la Mbunge kama jinsi ulivyoeleza ni kiasi cha Serikali kuhakikisha inapata marekebisho hayo ili kuweza kuyaangalia na kusema wanakubaliana nayo au hawakubaliani nayo. Huwezi ku-*rule out Amendment* ambayo Mbunge ameileta, kazi ya Mbunge ni kutunga sheria kwa *technicality* ambazo sio kosa la Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Kanuni za Bunge zizingatiwe, marekebisho niliyoyaleta yafanyiwe kazi kwa mujibu wa sheria.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu; Kanuni?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 88(1), kwa ruhusa yako Mwenyekiti naomba niisome inasema: "Mtoa hoja au Mbunge mwingine anayekusudia kuwasilisha mabadiliko katika Muswada unaojadiliwa, anaweza kumwomba Spika kwamba hatua ya kuingia katika Kamati ya Bunge Zima iahirishwe hadi wakati atakaoutaja katika ombi lake na Spika atatoa uamuzi wake kwa kadiri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umefafanua vizuri utata wa siku nyingi, ambao ulikuwa hauoneshi mipaka ya Katibu Mkuu.

Kamati ya Bunge Zima iahirishwe hadi wakati atakaoutaja katika ombi lake na Spika atatoa uamuzi wake kadiri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inasema kabla ya kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima; Mheshimiwa mtoa hoja hapa ni kwamba, tayari tumeshaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima, kwa hiyo, yuko nje ya kanuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kutukumbusha tena kuturejesha kwenye kanuni na ndiyo maana nilipomwambia Mheshimiwa Kabwe kwamba, nalazimika tuendelee kwa kuzingatia kwamba hili suala lilikuwa limechelewa, ilikuwa atusimamishe kabla hatujaingia kwenye hatua hii ya Kamati ya Bunge Zima halafu tuweze kutoa uamuzi utakaofaa kuhusiana na badiliko ambalo amelileta.

Mheshimiwa Zitto, usinyanyuke tafadhali! Hata hivyo, bado unayo nafasi kwa sababu tunafanya *Miscellaneous Amendment* katika Sheria mbalimbali hapa, unaweza kuleta katika utaratibu huo na litaangaliwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sijaomba Bunge lihairishwe na Wabunge wanaopiga kelele huko nyuma, wajue kwamba, mimi nimetumwa na watu waliosema ...

**MWENYEKITI:** Tafadhali ongea na Kiti.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Naongea na wewe ila nawapa salamu Wabunge kwamba ni jukumu langu kusema na *they have to keep quiet* kama hawana cha kusema.

Nafahamu kabisa kwamba, mabadiliko haya yana ukinzani mkubwa sana kwa sababu kwa muda mrefu sana, wanasiasa tumekuwa tuki-*enjoy* maslahi haya ya kuteuliwa kwenye Bodi mbalimbali za Wakurugenzi na mara nyingi mabadiliko yanakuwa ni tabu sana kukubalika.

Nilichokuwa nakiomba ni kwamba, lazima Wabunge tukubaliane na mabadiliko ambayo yanaendelea; suala hili limekuwa ni kero kubwa sana; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amekuwa akitoa mapendekezo haya.

Huu ni mwaka wa pili mfululizo, kwa hiyo ni jukumu letu kama Bunge, kuweza kuhakikisha kwamba, pale nafasi inapopatikana ya kuweza kufanya hayo marekebisho na ndio majukumu ya Mbunge kufanya ile *legislative function* ya kuweza kuleta hayo mabadiliko ambayo yanatakiwa.

*Reason* ya Serikali kwamba haina *Schedule of Amendment,* haina maana yoyote; kwa sababu kama nilivyosema hapo awali kwamba ni jukumu la Mbunge.

Ninachokubaliana na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, kuna taratibu mbalimbali za *Miscellaneous Amendments* na ni ushauri mzuri sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba *Miscellaneous Amendments* zitakazokuja, suala hili liwe *considered.* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa kuchukua ushauri wetu. Sasa tunaendelea kumalizia na sina haja ya kumwita Waziri au mwingine yeyote atoe ufafanuzi, kwa sababu maneno uliyomalizia ni mazuri tu.

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009**
***(The Executive Agencies (Amendment) Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia Muswada huu, kifungu kwa kifungu na kuupitisha pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Muswada umeshapitia hatua zake zote zinazotakiwa na sasa tunasubiri hatua ya mwisho kabisa, ambapo itatakiwa uende kwa Rais usainiwe iwe sheria na baada ya hapo utaanza kutekelezwa.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zote ambazo tulitakiwa tuzifanye siku ya leo zimekamilika; kwa maana hiyo, nachukua nafasi hii kutoa shukrani kwa ushirikiano tuliokuwa nao tokea asubuhi. Sasa naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 05.05 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 11 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*